



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU BENKI ZA TANZANIA
WOMEN'S BANK PLC, TANDAHIMBA COMMUNITY BANK LTD NA
KILIMANJARO COOPERATIVE BANK LTD**

Ndugu Wanahabari,

Kama mnavyofahamu, Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, imeipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kusimamia shughuli zote za kibenki na taasisi za fedha nchini kwa lengo la kuhakikisha uimara na ustahimilivu wa sekta ya kibenki na kifedha kwa ujumla.

Ikumbukwe kwamba, tarehe 4 Januari 2018, Benki Kuu iliziongezea muda wa miezi sita benki tatu ambazo ni Tandahimba Community Bank Limited (TACOBAL), Tanzania Women's Bank Plc (TWB) na Kilimanjaro Cooperative Bank Limited (KCBL) mpaka tarehe 30 Juni, 2018 ili kufikisha kiwango cha mtaji kinachohitajika na sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake cha kiwango cha chini cha mtaji cha shilingi bilioni 2 kwa benki za wananchi (community banks). Aidha benki hizo ziliongezewa muda wa mwezi mmoja hadi tarehe 31 Julai 2018 ili kukamilisha taratibu za kuongeza mtaji.

Napenda kuwafahamisha kwamba, sambamba na mkakati wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kurekebisha na kuboresha muundo wa benki za umma, wanahisa wa TWB and TPB wameamua kuunganisha benki hizi ili kuboresha ufanisi na utendaji wa benki hizo. Kufuatia muungano huo,

kutakuwepo na benki moja ambayo itaendelea kuitwa benki ya “TPB Bank Plc”.

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 30(1)(a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeridhia ombi la uunganishaji wa benki za TWB na TPB na kuwa benki moja kuanzia tarehe 03 Agosti 2018 itakayoendelea kuitwa benki ya “TPB Bank Plc” ambayo itaendelea kuwa na mtaji wa kutosha kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 17 cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Hivyo, wateja, wafanyakazi, mali na madeni yote ya benki ya TWB yataunganishwa na yale ya benki ya TPB.

Hivyo, muungano huu utafanya benki mpya ya TPB Bank Plc kuwa imara zaidi na itakuwa ina mtaji wa kutosha kama inavyotakiwa kisheria chini ya kifungu cha 17 cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

Benki Kuu inawaomba wateja wa benki ya TWB kuwa watulivu katika kipindi cha mpito cha uunganishaji wa benki hizi na waendeleo kupata huduma za kibenki kwa utaratibu utakaotolewa na menejimenti ya uongozi wa benki ya TPB.

Aidha, nichukue pia fursa hii kuwataairfu kuwa benki za TACOBANA na KCBL kwa sasa zimeweza kuongeza mtaji na kukidhi kiwango kinachohitajika kisheria na hivyo zinaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta uhimilivu katika sekta ya fedha.

BENKI KUU YA TANZANIA